

Maswali

1. Mungu alituma nini kuongoza watu wakati wa mchana?
2. Mungu aliwapa nini kuwaongoza wakati wa usiku?
3. Farao alifanya nini baada ya Waisraeli kuondoka?
4. Mbona Waisraeli waliogoba?
5. Nani aliamini Mungu?
6. Mungu alifanyaje nguzo la wingu?
7. Mungu aliambia Musa afanye nini?
8. Mungu alituma nini usiku kucha?
9. Waisraeli walivuka bahari namna gani?
10. Nini ilifanyika kwa Wamisri?

Majibu

1. Nguzo ya wingu.
2. Nguzo ya moto
3. Farao alibadilisha mawazo yake. Alituma jeshi lake kurudisha Waisraeli Misri.
4. Walikuwa katikati ya Wamisri na bahari. Walisahau kwamba Mungu atawasaidia.
5. Musa aliamini Mungu.
6. Mungu alibadilisha nguzo ya wingu ikarudi nyuma ili Wamisri wasione Waisraeli.
7. Mungu aliambia Musa anyoshe fimbo yake juu ya bahari.
8. Mungu alituma upepo wa nguvu uliovuma usiku kucha.
9. Waisraeli walivuka bahari kwa njia kavu iliyotengenezwa na upepo.
10. Wamisri walizama baharini.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



19 Waisraeli wavuka Bahari ya Shamu

Kwa Biblia Kutoka 13: 17-22 na mlango wa 14

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anajali watu wake wanaomtii. Mungu ana uwezo juu ya vitu vya asili.


Somo

Kutoka Gosheni ya Misri mpaka nchi ya Kanaani si mwendo mrefu sana. Njia fupi sana ni kupitia nchi ya Wafilisti. Wafilisti ni watu wa taifa kali tena katili. Mungu hakutaka watu wake wapitie njia hiyo.

Waisraeli walikua watumwa kwa miaka mingi. Mungu alijua kwamba itachukua muda mrefu kufanya Waisraeli wawe taifa la Nguvu. Mungu alitaka kufundisha watu wake juu ya sheria zake. Kwa hivyo Mungu aliambia Musa aongoze watu kupitia kwa changwa wakielekea Bahari ya Shamu. Mungu alituma nguzo ya wingu kuwaongoza Waisraeli mchana. Alituma nguzo ya moto kuwaongoza usiku. Kwa hivyo walifika Bahari ya Shamu.

Farao alikasirika baada ya watumwa wake Waisraeli kuondoka. Nani atafanya kazi yake yote ya kujenga? Wapelelezi wake wakamwambia, "Waisraeli wamepiga kambi karibu na Bahari ya Shamu. Hawawezi kuvuka maji, ukituma jeshi lako upesi utawashika."


Farao alituma magari yake ya kasi 600 kufuata Waisraeli. Baadaye akatuma magari mengine na jeshi lote la Misri. Akasema, "Tutawapata hao watumwa haraka."



Bunde si bunde, Waisraeli waliona Wamisri wamewafuata nyuma. Walikua wamenaswa katikati ya jeshi la Wamisri na Bahari ya Shamu. Waisraeli walikua na hofu. Walisahau kwamba Mungu alikua amewahidi kuwapeleka mpaka nchi ya Kanaani salama. Walisahau miujiza yote yenye Mungu alifanya walipokuwa Misri. Waisraeli walimkasirikia Musa na wakapasa sauti, "Mbona umetuleta tukufie huku? Ingekuwa vyema kama tukeendelea kuwa watumwa Misri."

Musa alijua kwamba Mungu atawaokoa. Aliamini Mungu. Aliwambia Waisraeli, " Msiogope. Nyamaza kimya na mtaona wokofu wa Bwana."

Musa aliomba Mungu na Mungu akajibu maombi yake. Mungu alitoa nguzo ya wingu mbele ya Waisraeli. Mungu aliiweka nyuma yao. Wamisri hawangeweza kuona Waisraeli kwa ajili ya wingu. Mungu akamwambia Musa anyoshe fimbo yake juu ya bahari. Musa alinyosha fimbo yake juu ya bahari na Mungu akaleta upepo wa nguvu sana kuvuma. Usiku mzima upepo ulivuma na kukawa na baridi nyingi. Upepo ulisukuma maji ya bahari. Upepo ulisanya maji na kuyagawanya. Ilipofika asubuhi kulikuwa njia kavu katikati.



Musa aliwambia, "Watu wangu, kujeni. Mungu ametutengenezea njia. Chukua mifugo na familia zenu na mnifuate." Watu wote na watoto wao na mifugo yao waliondoka wakitumia njia iliyogawanya maji. Walipita katikati ya bahari. Haikukuwa raisi. Upepo baridi ilikuwa bado inavuma. Njia ilikuwa na unyevu na mawe. Lakini Waisraeli walitumia hiyo njia na wakavuka n'gambo ya bahari salama.

Wingu lililokuwa nyuma ya Waisraeli lilitoka baharini. Wamisri walishangaa kuona njia katikati ya bahari. Farao alikasirika alipoona Waisraeli wameteoroka na kuvuka bahari. Farao alikadhabika. Alipasa sauti, "Watumwa wanatoroka. Lazima tuwafuate."

Watumwa
wanatoroka!



Farao aliamrisha magari na jeshi lake wafuate Waisraeli. Magari yalikimbia katikati ya kuta za maji kwa hiyo njia. Lakini magari yaligwama ndani ya mchanga nyepesi. Gurudumu zilin'goka kutoka kwa magari. Farasi waligwama kwa mchanga. Askari wa Misri waliogopa. Wakasema, "Turudi. Bwana Mungu ako anapigania Waisraeli. Hatuwezi kupigana na Bwana." Lakini muovu Farao hakurudi nyuma. Alitaka kuwashika Waisraeli watumwa.

Waisraeli walifika upande mwingine wa bahari salama. Waliona kwamba Wamisri walikua katikati ya bahari wanawafuata. Mungu alimwambia Musa anyoshe fimbo yake juu ya bahari. Musa alinyosha fimbo yake na kuta za maji zilikimbia kukuja pamoja. Wamisri hawangeokoka. Walipatikana katikati ya bahari. Farao na jeshi lake lote la Misri walizama.



Waisraeli waliokoka. Walimsifu Bwana Mungu. Waisraeli waliimba nyimbo za shukrani na kusifu Mungu. Wanawake walijeza na matari.